# NITAKUSHUKURU

ST. VERONICA - UMOJA 2
NAIROBI - KENYA.

ROBERT MURIUKI




Copyright ©R.MURIUKI 2012

ROBERT MURIUKI +254-722484855 rmuriuki2002@yahoo.com.

# NITAKUSHUKURU BWANA

1. Nitakushukuru Bwana milele
   Umenitendea  wema wa 'jabu
   Nitakusifu kwa nyimbo za shangwe

2. .Umenilisha na umeninywesha
   Wema wa  mbingu nimeupata
   Nashukuru Bwana u ndani yangu

***Nitakusifu,nikuimbie,***
***Nipige makofi kwa shangwe na nderemo  x2***

3. Ukarimu wako nahuruma yako
   Msamaha pia na upole wako
   Umenitendea wema wa ajabu

4. Ndani yangu kweli mwokozi yumo
   Hakika kwa mwili na Damu yake
   Ni rafiki yangu sitamwacha kamwe

5. Wema na fadhili zitanifuata
   Siku zangu zote za maisha yangu
   Nami  'ntakaa ndani yako daima

6. Nitalieneza jina lako Bwana
   Nilitangaze kwa mataifa yote
   Wakuinue na wakushukuru

***By:-Muriuki Robert***